

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

MKOA WA ARUSHA:

Anwani ya simu "REGCOM"

Simu Na. 2545608/2502289/2545870

Fax Na: 2545239 / 2544386

Barua Pepe: ras.arusha@tamisemi.go.tz

Barua Pepe: rasarusha@yahoo.com

Tovuti: www.arusha.go.tz



**OFISI YA MKUU WA MKOA,
S.L.P. 3050,
ARUSHA.**

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan tarehe 17/12/2016 aliagiza wananchi wote wafanye mazoezi ili kupambana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza, kama vile Shinikizo la damu, Kisukari, na Msongo wa mawazo. ***"Itengwe siku maalum kwa ajili ya wananchi wote kufanya mazoezi"***.

Katika kutekeleza agizo hili Mkoa wa Arusha kwa kushirikiana na vyama vya Michezo na wadau, umeandaa uzinduzi wa mpango huu kwa kila Wilaya tarehe 11/02/2017 wananchi wote watashiriki. Siku hii pia itakuwa na uzinduzi wa Kitaifa huko Dodoma.

Uzinduzi Kimkoa utafanyika katika Wilaya ya Arusha katika viwanja vya Sheikh Amri Abed kuanzia saa 12.30 Alfajiri hadi 6.00 Mchana na Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mheshimiwa Mrisho M. Gambo.

Aidha, Mkoa umeelekeza kila Wilaya kushirikisha Tarafa, Kata, Vijiji Vitongoji na Mitaa yote ili kila mwananchi apate fursa ya kushiriki mazoezi haya muhimu.

Mazoezi yatahusisha mchakamchaka (Jogging) kwa wananchi wote na kila Wilaya. Kauli mbiu ya Mkoa katika uzinduzi huu ni:- **"Shirika mazoezi, epuka magonjwa yasiyo ambukiza"**.

Mazoezi haya yatakuwa na TUZO katika ngazi ya Mkoa, Wilaya kila mwaka kwa kuzingatia ushiriki, ubunifu na idadi ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za Michezo.

Pamoja na hayo, Pia kutakuwa na zoezi la wananchi kupima afya zao na elimu kuhusu magonjwa hayo itatolewa.

Viongozi wote wa Taasisi za Umma, viongozi wa Tarafa, Kata na Mitaa wanaombwa kuwashirikisha wananchi wote katika zoezi hili muhimu. Viongozi wa michezo mbalimbali riadha, mpira, Klabu wanaalikwa kushirikisha wanachama wao katika zoezi hili.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha ataongea na wananchi na kushiriki uzinduzi huu.

Wananchi wote wa Mkoa wa arusha wanaombwa kujitokeza kwa wingi katika mazoezi haya ili kuanza kuimarisha afya kupitia mazoezi. Zoezi hili ni endelevu hivyo kila Jumamosi ya pili ya mwezi litafanyika.



Imeandaliwa na:

Ofisi ya Habari,

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Arusha

10/02/2017